

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE
07 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

Muda: Saa1:30

MAJIBU

Mwaka: 2015

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali yote.

maktaba.tetea.org



SEHEMU A: (Alama 20)

Soma swali na kisha chagua jibu lililo sahihi kati ya chaguzi nne ulizopewa na uandike herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku ulichopewa katika kila swali:

1. Simu ambazo hutumiwa na polisi ili kupeana taarifa zinaitwa

- A. simu za upepo
- B. simu za mkononi
- C. simu za mezani
- D. simu za intaneti

A. simu za upepo

Simu za upepo hutumiwa na vyombo vya ulinzi kama polisi kwa mawasiliano ya haraka.

2. Namba ya simu ambayo hutumiwa na watu kwenye matukio ya hatari kama moto ni

- A. 113
- B. 112
- C. 110
- D. 114

B. 112

112 ni namba ya dharura inayotumika katika matukio ya hatari.

3. Kifaa kipi kati ya vifuatavyo hutumika kutengenezea ngoma?

- A. Plastiki
- B. Kitambaa
- C. Ngozi
- D. Mwanzi

C. Ngozi

Ngozi hutumika kufunika ngoma ili kutoa sauti.

4. Kipande cha karatasi chenye maandiko yenye ujumbe maalumu ambacho hutumika kwa matangazo ya muda mfupi kinaitwa

- A. Bango
- B. Kipeperushi
- C. Gazeti
- D. Makala

B. Kipeperushi

Kipeperushi hutumika kutoa taarifa fupi kwa muda mfupi.

5. Kituo kipi kati ya vifuatavyo hutumika kutoa ushauri nasaha hapa Tanzania?

- A. ANGAZA
- B. SHIDEPHA
- C. WAMA
- D. EMAU

B. SHIDEPHA

SHIDEPHA ni kituo cha kutoa ushauri nasaha.

6. Nyumba au chumba kinachotunza vitabu na maandiko mengine kinaitwa

- A. Maktaba
- B. nyumba ya vitabu
- C. chumba cha vitabu
- D. stoo ya vitabu

A. Maktaba

Maktaba ni mahali rasmi pa kutunzia vitabu na maandiko.

7. Kipi kati ya vifuatavyo siyo chombo cha mawasiliano?

- A. Kamera
- B. Radio
- C. Luninga
- D. Magazeti

A. Kamera

Kamera hutumika kupiga picha, siyo chombo cha mawasiliano ya ujumbe.

8. Shirika la simu la Tanzania linalotoa huduma ya simu za mezani linaitwa

- A. Vodacom
- B. Tigo
- C. TTCL
- D. Nokia

C. TTCL

TTCL hutoa huduma za simu za mezani Tanzania.

9. Mwitiko maana yake ni hali ya upokeaji wa _____

- A. Ujumbe
- B. Maneno
- C. Maelezo
- D. Vitendo

A. Ujumbe

Mwitiko ni upokeaji wa ujumbe uliotumwa.

10. Neno au namba za siri ambazo humwezesha mtu kufungua kompyuta huitwa

- A. Kiteuzi
- B. Microsoft

C. Faksi

D. password

D. password

Password hutumika kama neno la siri kufungua kompyuta.

SEHEMU B: (Alama 10)

Katika swali la 11 hadi la 15 katika sehemu hii, chagua jibu sahihi kutoka Kifungu B kama yanavyoonekana kwenye jedwali, kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

Na.	Kifungu A	Herufi	Kifungu B
11.	Hutumika kupokea na kuchambua kazi zote zinazoingia kwenye kompyuta	(E)	E. Kichakato kikuu
12.	Hutumika kuchapa maandishi ya kompyuta kwenye karatasi	(D)	D. Printa
13.	Hutumika kuonyesha taarifa iliyomo ndani ya kompyuta	(F)	F. Skirini
14.	Hutumika kuingiza maelekezo kwenye kompyuta	(B)	B. Kibodi
15.	Hutumika kutoa sauti kwenye kompyuta	(C)	C. Spika

SEHEMU C: (Alama 05)

Katika swali la 16–20 andika KWELI kama sentensi hiyo inawasilisha maudhui sahihi, na SI KWELI kama sentensi hiyo inasilisha maudhui ambayo si sahihi.

16. Mayowe hutumika katika sherehe. **SI KWELI**

17. Alama za barabarani huonesha namna bora ya kutumia barabara. **KWELI**

18. Maandiko yanaweza kupangwa katika maktaba kulingana na mwandishi wa andiko.

KWELI

19. Filimbi ni njia ya kisasa ya mawasiliano. **SI KWELI**

20. Kompyuta nyingi hutumia programu andishi ya Microsoft Word. **KWELI**

SEHEMU D: (Alama 15)

Katika swali la 21–25, soma swali na uandike jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi:

21. Kifaa kinachotumika kuingiza umeme kwenye betri ya simu ya mkononi kinaitwa **chaja**.

22. Barua zimegawanyika katika mafungu mawili ambayo ni barua ya kirafiki na **barua rasmi**.

23. Hatua ya kwanza ya kutuma ujumbe kwa njia ya faksi ni **kuandaa ujumbe**.

24. Mchoro huu ufuatao huitwa **simu ya mezani**